JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

MUHTASARI WA TAALUMA YA KISWAHILI KWA STASHAHADA YA UALIMU NGAZI YA SEKONDARI

2009

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

MUHTASARI WA TAALUMA YA KISWAHILI KWA STASHAHADA YA UALIMU NGAZI YA SEKONDARI

2009

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi mwaka 2009

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuchapa au kutoa muhtasari huu kwa jinsi yoyote bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam
TANZANIA

'Tel': +255 222 773006, 277440
'Fax': +255 22 2774420
'E-mail': director@tie.go.tz

IDHINI

Kozi ya Ualimu wa Elimu ya Sekondari Ngazi ya Stashahada ni ya miaka miwili na imekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye moyo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule za sekondari. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu kozi ya miaka miwili ambapo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili limeidhinishwa rasmi kuwa ni **Muhtasari wa Taaluma ya Kiswahili kwa Stashahada ya Ualimu Ngazi ya Sekondari** wa mwaka 2009.

Umeidhinishwa na .....CHARLES PHILEMON.....

Saini.....cwPhilemon.....

Tarehe.....14 Septemba.....**2009**

/**Kamishna wa Elimu**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

S.L.P 9121

Dar es Salaam

Simu: +255 222 110150, 110179, 11046

Nukushi: +255 222 113271

Wovuti: www.moe.go.tz

YALIYOMO

Ukurasa

Utangulizi ……..……..... i

Maelezo kuhusu somo……..…….…… ii

Sababu za maboresho…….……...…….……iii

Malengo ya Jumla ya Kufundisha Kiswahili katika Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Stashahada ya Ualimu……..... iii

Ujuzi wa somo……..……..…….. iii

Malengo ya Kufundisha Taaluma ya Kiswahili katika Stashahada ya Ualimu Ngazi ya Sekondari ……..... iv

Mpangilio wa Muhtasari …….. iv

Upimaji ……..... v

Mada za Kitaaluma

1.0 Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili.....……..…..…..... 1

2.0 Matamshi na Lafudhi ……..…..……..... 4

3.0 Fasihi ……..……..... 4

4.0 Uhakiki wa Kazi za Fasihi ……..…… 6

5.0 Maendeleo ya Kiswahili ……..……..... 7

6.0 Ufahamu …….. 8

7.0 Uandishi ……..…….....10

Orodha ya Vitabu.....…….....12

UTANGULIZI

Muhtasari huu wa mwaka 2009 ni toleo la **Muhtasari wa Taaluma ya Kiswahili kwa Stashahada ya Ualimu Ngazi ya Sekondari** wa 2007 uliharirwa. Muhtasari huo ulikuwa na upungufu katika malengo ya jumla ya kufundishia Kiswahili katika Ualimu, Malengo ya kufundishia Kiswahili katika Stashahada Ngazi ya Sekondari, Maelezo ya somo, Muda wa kufundishia na katika vipengele kadhaa vya mada za kumwimarisha mwalimu mwanafunzi.

Uzoefu wa kutumia muhtasari huo umeonesha umuhimu wa kumuimarisha mwalimu mwanafunzi kitaaluma na kitaalamu. Sehemu hii inakidhi mahitaji ya kitaaluma ya wanachuo. Pia muhtasari huu unasisitiza ufundishaji na ujifunzaji shirikishi. Hii ina maana kwamba ufundishaji huu unamshughulisha mwanafunzi zaidi. Kwa msingi huu muhtasari huu unajikita kwenye ujenzi wa ujuzi anuai.

Somo la Kiswahili lina mihtasari miwili, mmoja wa taaluma na mwingine wa utaalamu. Kila muhtasari utafundishwa kwa saa mbili kwa wiki. Kwa hiyo mada za mihtasari ya Kswahili kwa taaluma na utaalamu zitafundishwa kwa saa nne katika wiki.

MAELEZO KUHUSU SOMO

Mafunzo ya somo la Kiswahili katika ngazi ya stashahada yanatarajiwa yawe ya miaka miwili. Katika kipindi hicho mwalimu tarajali atajifunza masomo ya kitaaluma na ya kitaalamu na kupata ujuzi katika masuala ya lugha, fasihi, njia na mbinu anuai katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika masuala mtambuko na ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Muda wa kila mada ndogo umeoneshwa. Muda huo ni makadirio tu. Mkufunzi, unaweza kurekebisha muda huo kulingana na mahitaji ya darasa lako. Kwa jumla inatarajiwa kuwa saa mbili zitatumika kila wiki kwa kufundisha muhtasari huu.

SABABU ZA MABORESHO

Mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari una malengo mbalimbali. Miongoni mwa malengo hayo ni kupata walimu bora. Aidha, dira ya elimu ni kuwaandaa walimu wenye taaluma bora na mwelekeo wake ni kutoa walimu wenye ujuzi wa kufahamu na kupima maendeleo ya wanafunzi na kutatua matatizo yao katika kujifunza. Zaidi ya hayo, tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari wanahitaji kuimarishwa katika utalaamu wa kufundisha darasani na kwenye taaluma ya lugha ya Kiswahili.

Kwa hiyo, muhtasari huu umeandaliwa ili kukidhi mahitaji ya taaluma yaliyotajwa hapo awali na kumwezesha mwalimu kulimudu vyema somo la Kiswahili.

MALENGO YA JUMLA YA KUFUNDISHA KISWAHILI KATIKA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA

Malengo ya jumla ya kufundisha Kiswahili katika vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada yanatarajiwa kuwa:

a) Kuelewa kuwa Kiswahili ni sehemu ya utamaduni wa Tanzania
b) Kuwa na tabia ya udadisi katika masuala ya lugha na fasihi ya Kiswahili.
c) Kujenga mwelekeo chanya katika kufundisha Kiswahili
d) Kuelewa vipengele mbalimbali vya taaluma ya somo la Kiswahili
e) Kujenga tabia ya kutumia Kiswahili fasaha katika Mawasiliano.
f) Kutumia Kiswahili kwa kuzingatia mwelekeo chanya kwenye masuala mtambuko na haki za binadamu.
g) Kutumia Kiswahili kuendeleza ujasiriamali.
h) Kuboresha welewa wa taaluma ya Kiswahili.

UJUZI WA SOMO

Baada ya kozi hii mwalimu mwanafunzi anatarajiwa apate ujuzi ufuatao:-

a) kuandika na kuzungumza Kiswahili kwa usahihi kwa kuzingatia ubunifu na kufikiri kwa makini..
b) kubaini, kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.

c) kuhakiki kazi za fasihi simulizi na za fasihi andishi kwa kuzingatia vigezo vya uhakiki na haki za binadamu.
d) kutunga kazi za fasihi simulizi na za fasihi andishi zinazoweza kuingiza kipato.
e) kubaini hatua mbalimbali za ukuaji na ueneaji wa Kiswahili nchini Tanzania na duniani kwa ujumla.

MALENGO YA KUFUNDISHA TAALUMA YA KISWAHILI KATIKA STASHAHADA YA UALIMU NGAZI YA SEKONDARI

Baada ya mafunzo ya ualimu, mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kutumia msamiati na miundo ya Kiswahili kwa usahihi katika maandishi na mazungumzo.
b) kutumia lafudhi ya Kiswahili kwa usahihi.
c) kubaini, kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi simulizi na za fasihi andishi
d) kutumia mbinu za kifasihi katika mazungumzo na maandishi.
e) kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili.
f) kueleza kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika enzi mbalimbali za kihistoria.
g) kutumia vifaa vyenye maudhui mbalimbali yakiwamo na masuala mtambuko na haki za binadamu katika kufundisha mada mbalimbali za Kiswahili.
h) kuboresha welewa wa taaluma ya Kiswahili kwa kiwango cha kidato cha sita.

MPANGILIO WA MUHTASARI

Muhtasari huu una sehemu mbili. Sehemu ya kwanza yenye kurasa za awali inajumuisha maelezo ya Mafunzo ya somo, sababu za mafunzo ya somo, malengo ya jumla ya kufundisha taaluma ya Kiswahili katika Stashahada, ujuzi wa somo, mpangilio wa muhtasari na upimaji, malengo ya kufundisha taaluma katika stashahada ya ualimu. saba

Sehemu ya pili ina maudhui ya kozi yanayojumuisha mada, malengo mahususi, mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa na taratibu za upimaji.

Muhtasari huu unazingatia mabadiliko na maendeleo katika utaalamu wa elimu. Aidha unamdokezea mkufunzi mambo anayotakiwa ayazingatie, lakini haumfungi kufikiri na kubuni mambo katika kuutumia. Kwa msingi huu muhtasari umeandikwa katika muundo wa maelezo yaliyotiririshwa.

Sehemu hii ina mtiririko wa:

a) Mada kuu
b) Mada ndogo
c) Malengo Mahususi
d) Mbinu za Kufundishia na kujifunzia
e) Zana za Kufundishia na Kujifunzia
f) Mbinu za upimaji

Muhtasari huu umekadiriwa kufundishwa kwa muda wa saa 128. Jumla hii inatokana na ukokotoaji ufuatao: Kila mwaka una miezi nane (8) ya mafunzo ya nadharia na miezi miwili (2) ya mafunzo ya vitendo. Miezi ya nadharia ina wiki 32 ambayo ikizidishwa kwa saa mbili kwa wiki tunapata saa 64 kwa mwaka. Kwa hiyo saa za nadharia ni 128 kwa miaka miwili. Saa hizo zimesambazwa kwenye mada ndogo ndani ya maudhui ya muhtasari huu.

.

Ni muhimu kukumbuka kuwa chini ya mada kuu kunaweza kuwa na mada ndogo moja au zaidi. Kila mada ndogo ina muda wa saa unaopendekezwa kutumiwa katika kujifunza malengo mahususi yanayotakiwa kufikiwa, mbinu za kufundishia na kujifunzia na zana za kufundishia na kujifunzia mada ndogo hiyo. Hata hivyo kuna sehemu chache ambazo hazikuwekewa mapendekezo ya zana. Mkufunzi anaweza kubuni zana zake, na mbinu za upimaji zinazofaa kupima utendaji wa mwanafunzi katika mada ndogo hiyo. Vile vile muda uliooneshwa ni makadirio tu. Mkufunzi anaweza kurekebisha muda kulingana na mahitaji ya darasa lake.

Muhtasari huu unamzingatisha mwalimu mwanafunzi kwenye mada kadhaa za mihtasari ya kidato cha kwanza hadi cha sita. Mada hizi zimeteuliwa ili zimsaidie kuimarisha taaluma yake.

Mkufunzi na uongozi wa chuo wahakikishe kwamba muhtasari huu unaandaliwa na unakidhi haja za wanafunzi wenye mahitaji maalum kama kutumia lugha ya alama na ishara kwa viziwi na herufi za vidutu (Breili) kwa wasioona.

UPIMAJI

Kwenye kila mada ndogo, kumewekwa mapendekezo ya namna ya kuwapima walimu wanafunzi katika mada ndogo hiyo. Upimaji huo unatakiwa uwe endelevu. Ni vema ufanyike kila baada ya mada ndogo kumalizika. Kwa ujumla upimaji umegawanywa katika mafungu mawili: wa kwanza ni upimaji endelevu unaoongozwa na mkufunzi na kupewa uzito wa 50% ya alama zote. Wa pili hufanywa na Baraza la Mitihani na unao uzito wa 50% ya alama zote.

Katika upimaji endelezi, mkufunzi anatarajiwa kuwapa wanafunzi wake majaribio manne ambayo alama zake zinasajiliwa. Hii ina maana ni jaribio moja kwa kila muhula litakalosajiliwa. Vilevile anatarajiwa awape wanafunzi wake kazi mradi tatu. Hii ina maana mbili kwa mwaka wa kwanza na moja kwa mwaka wa pili. Kutakuwa na upimaji wa kutumia mkoba wa kazi mara mbili. Mkoba wa kazi wa kwanza ni wa mwaka wa kwanza na ya pili ni ya mwaka wa pili. Kila muhula utakuwa na mtihani. Kwa hiyo kutakuwa na mitihani mitatu. Mitihani miwili ya mwaka wa kwanza itapewa alama 12 na mtihani wa muhula wa kwanza wa mwaka wa pili utapewa alama 8. Mgawanyo wa alama hizo unaonekana katika jedwali kama ifuatavyo:-

Namba	**Aina ya Upimaji**	**Fadaa**	**Uzito (%)**
	Upimaji Endelezi		**50%**
1.	Majaribio	4	5/5 (10)
2.	Kazi mradi	3	5/5 (10)
3.	Mkoba wa Kazi	2	5/5 (10)
4.	Mitihani ya Mihula	3	12/8 (20)
	Mtihani wa Mwisho (BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA)		**50**
	Jumla		**100**

Zana za kupimia zilizotajwa kama mazoezi, na majaribio ni mapendekezo. Mkufunzi anaweza kutumia zana nyingine anazoona zinafaa kuwapima walimu wanafunzi wake. Msisitizo hapa ni kwamba walimu wanafunzi wapimwe kadri ufundishaji unavyoendelea. Matokeo ya upimaji yafahamike kwa mwalimu mwanafunzi na yatumiwe kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

1.0 UTUMIZI WA MSAMIATI NA MIUNDO YA KISWAHILI

1.1 Kutumia maneno ya Kiswahili kwa usahihi (saa 8)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kufafanua aina za maneno ya Kiswahili.
b) kutumia aina za maneno ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Majadiliano ya vikundi, maswali na majibu na mazoezi kufafanua aina za maneno ya Kiswahili na matumizi yake.

Zana za kufundishia/kujifunzia

a) Kadi za maneno
b) Chati ya ukutani ya aina za maneno

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, majaribio mazoezi ya kuzungumza na mkoba wa kazi kupima kufafanua na kutumia aina za maneno.

1.2 Kutumia tungo za Kiswahili kwa usahihi (saa 4)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya tungo za Kiswahili
b) kueleza miundo ya tungo mbalimbali za Kiswahili.
c) kutumia tungo mbalimbali kwa usahihi katika mawasiliano.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Majadiliano ya vikundi, bungua bongo, maswali na majibu pamoja na mazoezi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Chati ya ukutani ya aina za tungo.

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, majaribio na mkoba wa kazi kupima welewa wa dhana na matumizi ya tungo.

1.3 Kuchambua sentensi za Kiswahili (saa 12)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kuainisha sentensi za Kiswahili.
b) kuchanganua sentensi za Kiswahili kwa njia za matawi na mishale.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Majadiliano ya vikundi, bungua bongo, maswali na majibu pamoja na mazoezi kuainisha na kuchanganua sentensi za Kiswahili.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Chati ya ukutani ya hatua za kuchanganua sentensi.

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, majaribio na mkoba wa kazi kupima uainishaji na uchanganuzi wa sentensi.

1.4 Utata katika mawasiliano (saa 5)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya utata katika mawasiliano
b) kufafanua chanzo cha utata katika mawasiliano.
c) kufafanua kwa mifano maana zinazojitokeza katika tungo tata.
d) kueleza jinsi ya kuondoa utata katika tungo.

e) Kufanya mazoezi ya kuondoa utata katika tungo.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Majadiliano ya jumla na ya vikundi, bungua bongo, mazoezi na igizo kueleza dhana ya utata, vyanzo vya utata na maana zinazotokana na tungo tata.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Chati ya maneno au tungo zenye maana zaidi ya moja.

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, majaribio na mkoba wa kazi na kazi mradi kupima dhana ya utata wa tungo, chanzo cha utata na jinsi ya kuondoa utata katika tungo.

1.5 Kutumia kamusi (saa 12)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze kubaini maana, aina na matumizi ya maneno kwa kutumia kamusi.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

a) Mbinu za mihadhara mifupi, majadiliano ya vikundi, onesho mbinu na mazoezi kubaini maana, aina na matumizi ya maneno kwa kutumia kamusi na mazoezi ya kupanga maneno ki-kamusi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Kadi za maneno na kamusi.

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, mazoezi ya kusoma kamusi, mazoezi ya kupanga maneno ki-kamusi, mkoba wa kazi na kupima matumizi ya kamusi.

2.0 MATAMSHI NA LAFUDHI YA KISWAHILI

2.1 Kutumia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili (saa 6)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kutamka maneno ya Kiswahili kwa usahihi.
b) kutumia lafudhi sahihi ya Kiswahili katika mawasiliano.
c) kusahihisha makosa ya matamshi na lafudhi ya Kiswahili katika hotuba.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Igizo dhima, onesho mbinu, majadiliano ya vikundi, kutunga hotuba na kuiwasilisha darasani na mazoezi kufundisha kutamka maneno na sentensi za Kiswahili kwa usahihi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

a) Redio na kanda za sauti zilizorekodiwa.
b) Mchoro unaoonesha ala za sauti za binadamu.

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuzungumza (kutamka), mkoba wa kazi, uchunguzi wa matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili na kupima welewa wa matamshi na lafudhi.

3.0 FASIHI

3.1 Kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi (saa 6)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza maana ya fasihi
b) kueleza umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.
c) kuainisha njia mbalimali za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.
d) kueleza ubora na udhaifu wa mbinu/njia mbalimbali za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.
e) Kukusanya kazi za fasihi simulizi na andishi.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Kazi-mradi, majadiliano na kueleza maana, umuhimu, njia za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

a) Tepu rekoda (kinasa sauti)
b) Kalamu, karatasi
c) Kanda za sauti
d) Kanda za video
e) Kamera

Mbinu za Upimaji

Kazi mradi, uandishi wa ripoti, mazoezi ya kuandika, testi na mkoba wa kazi kupima welewa katika kukusanya, kuhifadhi na utambuzi wa udhaifu wa njia mbalimbali za kuhifadhi fasihi.

3.2 Kutunga kazi za fasihi (saa 14)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kubaini kanuni za utunzi wa kazi mbalimbali za fasihi.
b) kutunga kazi mbalimbali mashairi, riwaya na tamthiliya.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Majadiliano ya jumla na ya vikundi kubaini mbinu za utungaji wa kazi za fasihi. Onesho mbinu, kazi mradi na mazoezi ya kutunga hadithi, riwaya, mashairi na ngonjera. Wanachuo wafanye mazoezi ya kughani mashairi, kuigiza tamthiliya na kuwasilisha riwaya walizotunga.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Matini za kazi za ubunifu

Mbinu za Upimaji

Kazi-mradi na vilawa vyake, mazoezi ya kuandika na mkoba wa kazi kupima utungaji wa kazi za fasihi.

4.0 UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI

4.1 Misingi ya uhakiki (saa 4)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya uhakiki
b) kubaini misingi ya kuhakiki kazi za fasihi.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Bungua bongo, mihadhara mifupi, majadiliano ya jumla na ya vikundi na mazoezi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Chati ya ukutani ya vipengele vya fani na maudhui

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, majadiliano ya vikundi, mazoezi ya kuzungumza, testi na mkoba wa kazi kupima dhana na misingi ya kuhakiki kazi za fasihi

4.2 Kuhakiki kazi za fasihi (saa 16)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

Kuhakiki mashairi, riwaya na tamthliya kwa kufuata misingi ya uhakiki.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Tumia majadiliano na mazoezi kuhakiki kazi za fasihi. Vitabu, magazeti na majarida anuai.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Matini mbalimbali na vitabu mbalimbali

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, majaribio na mkoba wa kazi na kazi mradi kupima uhakiki wa kazi za fasihi.

5.0 MAENDELEO YA KISWAHILI

5.1 Asili ya Kiswahili (saa 10)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza chimbuko la Kiswahili kwa kutumia ushahidi wa kihistoria.
b) kuonesha ushahidi wa kimsamiati na kimuundo kuhusu ubantu wa Kiswahili.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Tumia majadiliano, bungua bongo na mazoezi kueleza chimbuko la Kiswahili, mgeni mwalikwa na mazoezi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Ramani ya Afrika kuonesha mtawanyiko wa Wabantu.

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, kazi mradi, uandishi wa ripoti na mkoba wa kazi kupima welewa wa dhana ya ubantu wa Kiswahili.

5.2 Kukua na kuenea kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki (saa 8)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

b) kueleza mambo yaliyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki Kabla ya Uhuru.
c) kutaja na kuelezea vyombo mbalimbali vinavyokuza na kueneza Kiswahili tangu kupata uhuru.
d) kueleza mafanikio na matatizo yanayovikumba vyombo vinavyokuza na kueneza Kiswahili katika Afrika Mashariki.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Majadiliano, bungua bongo, ziara na kazi mradi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Ramani ya Afrika Mashariki kuonesha misafara ya kibiashara.

Mbinu za Upimaji

Kazi mradi, uandishi wa ripoti, mazoezi ya kuandika na mkoba wa kazi kupima welewa wa kukua na kuenea kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki.

6.0 UFAHAMU

6.1 Ufahamu wa kusikiliza (saa 6)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya ufahamu wa kusikiliza.
b) kubaini mawazo makuu kutokana na habari aliyosikiliza
c) kueleza maana za maneno na misemo kama ilivyotumika kwenye habari aliyosikiliza.
d) kujibu maswali yatokanayo na habari aliyosikiliza.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Mihadhara mifupi, majadiliano na mazoezi.

Zana Mbinu za kufundishia/kujifunzia

a) redio
a) matini
b) magazeti

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, na mkoba wa kazi.

6.2 Ufahamu wa kusoma (saa 6)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya ufahamu wa kusoma
b) kubaini mawazo makuu kutokana na habari iliyosomwa
c) kueleza maana na misemo kama ilivyotumiwa kwenye habari/matini iliyosomwa.
d) kujibu maswali kutokana na habari aliyosoma

Mbinu zinazopendekezwa

Mihadhara mifupi, majadiliano na mazoezi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

a) Matini
b) Magazeti
c) Vijarida

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kuzungumza, majaribio na mkoba wa kazi.

6.3 Ufupisho wa Habari (saa 4)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya ufupisho
b) kufafanua misingi ya ufupisho wa habari
c) kufupisha habari aliyosikiliza au aliyosoma kwa kuzingatia misingi ya kufupisha habari.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Mihadhara mifupi, maswali na majibu, majadiliano ya jumla na ya vikundi na mazoezi katika kufundisha ufupisho wa habari.

Zana za kufundishia/kujifunzia

Matini iliyofupishwa

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kusikiliza na kuzungumza, majaribio na mkoba wa kazi kupima misingi na ufupishaji wa habari.

7.0 UANDISHI

7.1 Uandishi wa insha: Saa 10

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza dhana ya uandishi wa insha
b) kufafanua aina za insha
c) kufafanua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.
d) kuandika insha kwa kuzingatia muundo wa insha na masuala mtambuko.

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Mihadhara mifupi, kazi mradi, majadiliano, majadiliano ya vikundi, bungua bongo na mazoezi.

Zana za kufundishia/kujifunzia

a) Matini za mifano ya insha

b) Kielelezo cha muundo wa insha

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, majaribio, kazi mradi na mkoba wa kazi kupima misingi na uandishi wa insha.

7.2 Uandishi wa hotuba (Saa 6)

Malengo Mahususi

Mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kueleza maana ya hotuba
b) kufafanua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba.
c) kuandika hotuba kwa kuzingatia mada za masuala anuai ya jamii yakiwemo masuala mtambuko..

Mbinu za kufundishia/kujifunzia

Mihadhara mifupi, majadiliano, majadiliano ya vikundi, onesho mbinu na mazoezi ya kufundisha uandishi wa hotuba na igizo.

Zana za kufundishia/kujifunzia

a) Matini ya mfano wa hotuba
b) Hotuba iliyorekodiwa

Mbinu za Upimaji

Mazoezi ya kuandika, mazoezi ya kusikiliza na kuhutubia na mkoba wa kazi kupima misingi na uandishi wa hotuba.

OORODHA YA VITABU

1. Gibbe, A na Mvungi, T.A (1989); ***Fasihi Simulizi Sekondari na Vyuo,*** Standard Publishers, Dar es Salaam, Tanzania.

2 Kapinga, M.C (1983); ***Sarufi Maumbo ya Kiswahili,*** TUKI, Dar es Salaam.

3. Mmalavi, A.P.W. (1997); ***Lugha Katika Jamii***, East Afrian Publishing House, Nairobi, Kenya.

4. Mnyampala na Chiraghdin (1959); ***Historia ya Kiswahili,*** O.U.P, Dar es Salaam, Tanzania.

5. Msokile M. (1992); ***Historia na Matumizi ya Kiswahili,*** Educational Publishers and Distributors Ltd, Dar es Salaam, Tanzania.

6. Mwangomango, J.S.M. na Maganga, C, (1991); ***Mazoezi Fasaha ya Kiswahili***, DUP, Dar es Salaam, Tanzania.

7. Nkwera, F.V. (1979); ***Safuri na Fasihi Sekondari na Vyuo***, T.P.H Dar es Salaam

8. Sengo, T.S.Y. et al (1987); ***Uhakiki wa Vitabu vya Fasihi Sekondari na Vyuo,*** Nyanza Publications Agency, Dar es Salaam, Tanzania.

9. Senkoro F.EM.K (1998); Ushairi: ***Nadharia na Tahakiki***, DUP, Dar es Salaam, Tanzania.

10. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1983); ***Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili JUZUU ya 1 hadi ya 3,*** TUKI, Dar es Salaam, Tanzania.

11. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Zanzibar (1981); ***Misingi ya Nadharia ya Fasihi*** TAKILUKI, Zanzibar.

12. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988); ***Kiswahili Sekondari,*** TAUMI, Dar es Salaam, Tanzania.

13. Taasisi ya Elimu Tanzania (1996); ***Kiswahili Kidato 1, 2, 3 na 4,*** Oxford University Press, Dar es Salaam, Tanzania

14. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Zanzibar (1990); ***Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kidato cha Kwanza,*** TAKILUKI, Zanzibar, Tanzania.

15. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, ***Mulika***, Matoleo mbalimbali.

16. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Tanzania (1989); ***Kiswahili Vyuoni,*** TAUMI,

Dar es Salaam

17. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1981), ***Kamusi ya Kiswahili Sanifu,*** Oxford University Press, Dar es Salaam, Tanzania.

18. Whiteley, W. (1970); ***Swahili: The rise of a National Language,*** O.U.P, Dar es Salaam.

Angalia pia wovuti mbalimbali za tasnia ya Kiswahili hasa za Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Taasisi ya Elimu Tanzania, na nyinginezo. Ukiandika majina ya taasisi hizo kwenye injini za kutafuta habari kwenye mtandao wa intaneti basi wovuti hizo zitajitokeza.